Advance your carrier, enhance learning

# VICTORY HEALTH AND ALLIED SCIENCES COLLEGE

P. O. Box 121 – TABORA

**NACTE REG/HAS/209**

Web: www.vihasco.ac.tz E-mail: vihasco@yahoo.com, phone: +225 626 579 274/ +225 623771 943

**YAH:KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA STASHAHADA(DIPLOMA) YA FAMASIA MUHULA WAMASOMO SEPTEMBER.2022/2023**

Ndugu,……………………………………..…………………………………………………

Ninayo furaha kukujulisha kuwa, umechaguliwa kujiunga na chuo cha Victory Health and Allied Sciences College katika fani ya Famasia kwa ngazi ya Diploma, Chuo kipo Tabora mjini Eneo la Inala barabara ya kuelekea Dares salaam kutokea Tabora mjini ni mwendo wa kilometa 20.

## 1. MUDAWAKUFUNGUACHUO

Muda wa kufungua chuo ni kuanzia tarehe 03/10/2022, hivyo utatakiwa kufika chuoni kuanzia tarehe hiyo mpaka tarehe 18/10/2022 kwa ajili ya kuanza masomo

## 2. MAELELEZO YA JUMLA WAKATI UNAFIKA CHUONI

1. Ada Inapolipwa haitarudishwa ama kuwekwa kwaajili ya mwaka mwingine wa masomo,au kuwekwa kwa ajili ya matumizi mengine hivyo fanya maamuzi sahihi ya kulipa ada kwaajili yamasomo.
2. Hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kuingia darasani bila kufanya malipo ya ada pamoja na michango kama ilivyoelekezwa au kuonyesha ushahidi kutoka kwa mfadhili..
3. Pesa ya mitihani iliyoelekezwa ni kwaajili ya mwaka wa masomo 2022/2023

## 3. SHERIA , TARATIBU ZACHUO NA SERA ZA MITIHANI

Kila mwanafunzi atapatiwa nakala ya sheria, taratibu na sera za chuo siku chache baada ya kufika chuoni. Kila mwanafunzi atatakiwa kuisoma na kala hiyo kwa ufasaha kwakuwa utoa maelekezo na miongozo ya kipindi atakapokuwa chuoni. Na haya ni baadhi ya makosa ya nayoweza kukufanya usiendelee kuwepo chuoni kwa kufukuzwa.

- Wizi,uasherati,namatumizi ya madawa ya kulevya
- Kuharibu mali za chuo
- Ugomvi
- Kufeli masomo (Kutofikia wastani wa ufaulu katika masomo kulingana miongozo)
- Utoro wa bila taarifa
- Migomo

## 4. USAJILI

Utatakiwa kufika ofisi ya Udahili pale unapofika chuoni ili kukamilisha usajili na utunzaji wa kumbukumbu, Ikiwa umefika chuoni nje na muda wa kazi tafadhali piga simu namba 0626579274 uweze kupatiwa msaada.

Utatakiwa kuonesha vitu vifuatavyo

1) Vyeti halisi au nakala ya matokeo sawa na idadi uliyofanya mitihani ya kidato cha nne au cha sita. Nakala za mitihani (Result slip) zitakazokubaliwa ni zile zawanafunzi waliomaliza kidato cha nne mwaka 2021
2) Vivuli vya vyeti Hivyo kwa ajili ya matumizi ya ofisi
3) Picha nne (4) (passport size)
4) Risitiza benki zinazothibitisha malipo ya ada na michango uliyoyafanya
5) Joining Instruction na Application form zilizojazwa kwa ajili ya kutunza kumbukumbu
6) Wanafunzi wanaotoka nje ya Tanzania wanatakiwa kuonesha kibali cha usafiri (passport)
7) Cheti cha kuzaliwa
8) Fomu ya kupimwa iliyothibitishwa na Daktari kutoka kituo chochote cha afya kinachotambuliwa na serikali

Usijaribu kuonesha taarifa za uongo kwani kufanya hivyo ni kinyume na sheria jambo litakaloweza kukufanya ufikishwe kwenye vyombo vya sheria

## 5. MALAZI

Chuo kinatoa sehemu ya kulala kwa wanafunzi wote bila kujali mwanafunzi anatokea wapi isipokuwa kwa wale wenye sababu maalumu za kukaa nje na bweni za chuo ambazo zimedhibitishwa na mkuu wa chuo. Mwanafunzi atatakiwa kulipia ada ya malazi kama ilivyoelekezwa katika mchanganuo wamalipo kabla ya kuruhusiwa kulala ndani.

Mwanafunzi atatakiwa kufika na vitu vifuatavyo kwa ajili ya matumizi yake binafsi na malazi Godoro dogo lenye upana wa futi 3 na urefu wa futi 6, Mashuka mawili (rangiyoyote), blanket, Taulo, Ndala, Neti na ndoo.

## 6. SAREZACHUO

Wanafunzi wote watatakiwa kuvaa sare za chuo kama zilivyopendekezwa na uongozi wa chuo, Sare kwa wanafunzi wote utolewa chuoni siku chache baada ya wanafunzi kuripoti, sare zinazotolewa ni gauni 1 nyeupe na koti ya maabala kwa wasichana na Suruali moja ya kaki, shati 1 nyeupe na koti ya maabala kwa wavulana, mwanafunzi atatakiwa kujana viatu vya chini vilivyofunikwa vyenye rangi nyeusi na soksi nyeupe.

Nguo za nyumbani zinazoendana na maadili ya Kitanzania zinaruhusiwa baada ya muda wa masomo

## 7. CHAKULA

Chuo kina mgahawa ambao utoa huduma ya chakula kwa bei ndogo ambapo mwanafunzi anaweza kulipia shilingi za Kitanzania 120,000/= kwa mwezi au kwa kununua mwenyewe kila siku, Pesa ya chakula aitalipwa chuoni bali kwa mzabuni wa chakula.

## 8. MUHIMU

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na rimu 4 kwa mwaka
Zenye ukubwa wa A4 ambapo anaweza kuleta mbili(2) anaporipoti chuoni nanyingine mbili zitaletwa wakati wa kuanza muhula wapili. Madaftari, kalamu,rula,penseli, seti ya mahesabu (mathematical set), taulo ndogo mbili kwa ajili ya maabara, box moja la (Examination gloves) na scientific mathematical calculator moja.

## 9. MCHANGANUO WA ADA NA MICHANGO MINGINE

| **Maelezo** | **Mwanzoni mwa muhula wa kwanza (October2022)** | **Miezi miwili baada ya muhula wa kwanza (December2022)** | **Mwanzoni mwa muhula wa pili (march 2023)** | **Miezi miwili Baada ya muhula wa pili (may 2023)** | **Jumlaya Ada na michango itakayolipwa** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ada (karo)** | **400,000** | **350,000** | **400,000** | **350,000** | **1,500,000** |
| Usajili wa NACTE | 20,000 | - | - | | **20,000** |
| NACTE Quality Assurancefee | 15,000 | | | | **15,000** |
| Mitihani ya wizara | | | 150,000 | | **150,000** |
| Mitihani ya ndani (VIHASCO) | 100,000 | | | | **100,000** |
| Umoja wa wanafunzi | 5,000 | | | | **5,000** |
| Tahadhari | 50,000 | | | | **50,000** |
| Kitambulisho | 10,000 | | | | **10,000** |
| Sare ikihusisha LabCoat | 70,000 | | | | **70,000** |
| Tisheti | 10,000 | | | | **10,000** |
| **Jumla ndogo** | | | | | **1,930,000** |
| Malazi/Hostel | 45,000 | 45,000 | 45,000 | 45,000 | **180,000** |
| Jumla kuu | **725,000** | **395,000** | **595,000** | **395,000** | **2,110,000** |

## 10. MICHANGOMINGINE

| **Maelezo** | **KIASI** | **MUHUSIKA** | **MUDA** |
|---|---|---|---|
| Vitabu vya Mazoezi/TPH | 50000 | Wote | Mwaka wa kwanza mwishoni mwa muhula wa Kwanza(February 2023) |
| Matibabu/Bima | 50400/= | Wasiokuwa na bima ya Afya | Kila mwaka mwanzoni mwa muhula wakwanza |
| Field | 150,000/= | Wote | Kila mwaka mwishoni mwa muhula wa kwanza |

- Malipo yote yaliyoorodheshwa katika kipengele cha Ada na michango kulingana na awamu yalipwe kabla ya kuripoti chuoni kupitia **AKAUNTI YA BENKI NAMBA;**

***NMB: 51010074169*** *Jina* ***VICTORY HEALTH AND ALLIED SCIENCES COLLEGE-TABORA***

**UTHIBITISHO**
Mimi,________________________________Ninathibitisha kwamba kwa akili yangu timamu nimesoma na kuelewa fomu ya maelezo ya kujiunga na chuo cha Victory Health and Allied Sciences College na ninaahidi kufuata maelekezo kama yalivyoelekezwa.
Sahini………………………………..Tarehe………………………..

Tunakutakia maandalizi mema ya kujiunga nasi, karibu Victory Health and Allied Sciences College kwa Elimu bora na yenye mafanikio.

**Wako**

**…………………..**

**FELISTER JOSEPH**

**(MKUU WA CHUO)**

VICTORY HEALTH AND ALLIED SCIENCES COLLEGE
**P. O. Box 121 – TABORA**
**NACTE REG/HAS/209**

Advance your carrier, enhance learning

Web: www.vihasco.ac.tz E-mail: vihasco@yahoo.com, phone: +225 626 579 274/ +225 623771 943

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

FULL NAME ………………………………………………………………………..

Please check the above named to his/her physical and mental fitness:

Eyesight……………………………………………………………………………………........................

Hearing……………………………………………………………………………………..............................

Limbs……………………………………………………………………………………..............................

Speech……………………………………………………………………………………............................

Venereal diseases/STD…………………………………………………………………………...............

Leprosy……………………………………………………………………………………......................

Epilepsy……………………………………………………………………………………....................

Neurosis……………………………………………………………………………………....................

Diabetic mellitus........................................................................................................................

Tuberculosis..............................................................................................................................

Hemoglobin Level.........................................................................................................................

Pregnancy......................................................................................................................................

Any other deformity (specify)........................................................................................................

Other seriousdisease (specify)......................................................................................................

He/she is physically fit/unfit to follow this course

Approved by

…………………………………………………Signature……….............Date .................. /22

Station:……………………………………..Stamp.....................